BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

**KWA BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

***Mheshimiwa Spika;***

Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea na shughuli za Baraza.

***Mheshimiwa Spika;***

Pia, ninakushukuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako wote kwa kutuongoza vyema katika shughuli zetu za Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio waliotuwezesha kufika hapa kwenye chombo hiki adhimu.

***Mheshimiwa Spika;***

Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu uaminifu na uadilifu ili kuhakikisha kuwa mipango ya Serikali inatekelezwa kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi na kuimarisha maisha ya wananchi.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati inaomba kutoa shukrani zake za dhati kwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Mheshimiwa Riziki Pembe Juma pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hii Ndugu Joseph Kilangi na wakurugenzi mbali mbali kwa juhudi zao na mashirikiano yao makubwa wanayoipatia Kamati yetu wakati wote wa kazi zake.

***Mheshimiwa Spika;***

Shukrani za pekee ziende kwa wajumbe wa Kamati hii ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kazi nzuri wanayoifanya katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa mnasaba huo, naomba sasa kuwatambulisha wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla — Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Foum Mussa — Mjumbe
4. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed — Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe — Mjumbe
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Mjumbe
7. Mhe. Rukia Omar Ramadhan — Mjumbe

Aidha, Kamati hii ina makatibu wawili ambao hatuna budi kuwashukuru kwa kutekeleza majukumu kitaalamu na kwa ufanisi mkubwa. Makatibu wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni, na
2. Ndg. Ali Alawy Ali.

***Mheshimiwa Spika;***

Baada ya utangulizi huo na kwa kutumia Kanuni ya 107(3) Jadweli la kwanza ambalo limetupa jukumu la kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kazi ambayo kwa kadiri ya uwezo wetu tumejitahidi kuifanya kwa kufuatilia kiundani kabisa Utekelezaji wa Taasisi zote zilizochini ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya

Makaazi, katika vipindi tofauti ili kuhakikisha kuwa Dira na Malengo ya Serikali yanatekelezwa kwa kufuata Mipango ya Serikali, Ilani ya ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020/2025 kwa pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050.

***Mheshimiwa Spika;***

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi yenye **Fungu N02** inatekeleza majukumu yake kwa kutumia Programu kuu *Tatu (3)* na Programu ndogo Tano (*5)* ambazo zinasimamiwa na Idara mbali mbali zilizochini ya Wizara kwa dhamira ya kutoa mchango wa hali ya juu katika ustawi wa Taifa kupitia matumizi bora na endelevu ya rasilimali ardhi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

***Mheshimiwa Spika;***

Katika utekelezaji wa Programu Kuu hii ya ***Usimamizi wa Ardhi na Makaazi*** ina inajukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na huduma za makaazi bora kwa wananchi. Katika program ndogo ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ambayo inasimamiwa na Mahakama ya Ardhi kwa lengo la kupokea, kusikiliza na kuamua kesi za migogoro ya ardhi katika maeneo yote Unguja na Pemba, Kamati yetu imebaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali ambazo zinaifanya Mahakama ya Ardhi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kutofikia malengo yake. Uhaba wa fedha za matumizi, ukosefu wa vitendea kazi na uhaba wa Mahakimu ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazorudisha nyuma utelekezaji wa program hii.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati inashauri katika kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuimarisha matumizi na umiliki halali wa ardhi, Serikali iangalie kwa jicho la huruma umuhimu wa Taasisi hii yenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi ambayo imedumu kwa kipindi kirefu kwa kupatiwa Mahakimu wa kutosha pamoja na fedha za kutosha zitakazosaidia kutekeleza majukumu yao.

***Mheshimiwa Spika;***

Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni ya Ardhi kupitia program hii Kamisheni imeweza kutekeleza vyema shughuli zake na kufanikiwa kukusanya mapato yake kwa asilimia 97.5 ya makadirio. Kamati inashauri licha ya makusanyo mazuri yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka uliopita, pia uwepo Utaratibu madhubuti wa utoaji wa hati za matumizi ya ardhi ili kuepusha mrundikano mkubwa wa wananchi wanaoomba kupimiwa na kupatiwa hati zao kwa mujibu wa sheria.

***Mheshimiwa Spika;***

Katika program ndogo ya ***Utawala wa Ardhi, Nyumba na Makaazi*** ambayo imelenga kuhakikisha usalama wa umiliki wa Ardhi na uimarishaji wa huduma za makaazi kupitia upimaji wa ardhi, utambuzi na usajili wa ardhi, mipango miji na matumizi ya ardhi, ukarabati wa nyumba za maendeleo na majengo ya kihistoria,

Kamati imebaini kuwepo kwa baadhi ya watu ambao wamepatiwa hati za matumizi ya ardhi kwa lengo la makaazi na badala yake wanabadilisha matumizi yake na kufanya matumizi ya kibiashara kama vile hoteli au ujenzi wa nyumba za kibiashara. Kamati inashauri ili kudhibiti matumizi halali ya ardhi basi uwepo ufuatiliaji wa kina kwa watu wanaoleta maombi ya hati na msisitizo zaidi uwepo kwa wageni wanaokuja kwa lengo la uwekezaji.

***Mheshimiwa Spika;***

Kupitia Shirika la Nyumba Zanzibar, Kamati ilifanya ziara maalum ya kuzitembelea nyumba za maendeleo Unguja na Pemba na kuona changamoto mbali mbali ambazo zimejitokeza katika maneo hayo. Changamoto nyingi ambazo zinajitokeza zinasababishwa na wananchi ambao wanatumia nyumba za Shirika ikiwemo kuvunja na kubadilisha matumizi ya nyumba husika. Vile vile, nyumba ambazo wananchi walipewa kama fidia wamekuwa mstari wa mbele katika kufanya mabadiliko na kusababisha uharibifu katika nyumba hizo na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi yao. Kamati inashauri Serikali kupitia Shirika la Nyumba na Mamlaka zinazohusika na udhibiti wa makaazi kuhakikisha wamefuatilia kwa kina matumizi ya nyumba hizi kama ilivyokuwa katika malengo ya Muasisi wa Mapinduzi kwa wananchi wetu.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati inasikitishwa na hali ya uendeshaji wa Shirika la Nyumba kwa ujumla kutokana na kutofikia malengo iliyojipangia, hali hii inatokana na kiwango kikubwa cha madeni ambayo wanadai kutoka kwa wateja wake kuanzia miaka ya 1990 hadi sasa ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2021 Shirika linadai jumla ya **shilingi 1,880,429,000** kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni **shilingi 248,521,000.**

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati pia imebaini kuwepo kwa tatizo la muhali juu ya ulipaji wa madeni ya nyumba kwa wateja wake ambao Shirika linashindwa kuwachukulia hatua kwani wapo baadhi ya wadaiwa hukingiwa vifua na wakubwa na kupelekea ugumu katika ukusanyaji wa kodi kitu ambacho kinapelekea Shirika kushindwa kufikia malengo yake katika ukusanyaji wa mapato.

Hivyo, Kamati inashauri kupitia Shirika la Nyumba kusimamia kikamilifu wateja wote ambao wanadaiwa na Shirika ili kulipa madeni yao na kuongeza mapato ya Shirika kwa ujuml. Kwani kuwepo kwa madeni hayo kunapelekea kukosekana kwa fedha za matumizi na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mipango ya Shirika katika ujenzi wa nyumba mpya na matengenezo ya nyumba ziliopo ukizingatia Shirika hili halipokei ruzuku yoyote kutoka Serikalini.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati pia imejuilishwa kuwa uwepo wa kodi ndogo za nyumba ambazo haziendani na bei ya soko iliyopo inapelekea Shirika kushindwa kuzifanyia matengenezo nyumba zake na kubaki kuwa chakavu na hatarishi kwa muda mrefu kutokana na mapato madogo ya makusanyo. Hivyo basi, kamati inashauri Serikali kuridhia kupandishwa kwa kodi ya nyumba kwa kiwango ambacho kitaendana hali ya wananchi ili basi Shirika lipate angalau kuweza kujiendesha lakini pia kuweza kuongeza mapato

ambayo wataweza kuyatumia katika kufanya matengenezo nhyumba zilizochakaa kwa ajili ya kuzikinga na kuepeka kuleta athari kwa maisha ya watumiaji wa nyumba hizo.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati inasisitiza kuchukuliwa hatua kwa wale wote wanaofanya uharibifu wa nyumba zinazomilikiwa na Shirika kwa kuzibadilisha matumizi yake na kuzifanya zakibiashara kwa kuweka milango ya maduka sehemu ya chini ya nyumba hizo pamoja na kuzibadilisha uhalisia wake kwa kuzibomoa na kuzifanyia ukarabati ambao unaathiri uimara wa nyumba zenyewe. Kamati inapendekeza kuwa Shirika litafute dalali ambaye atasaidia katika kusimamia na kushughulikia madeni yao badala ya kuwatumia ZAECA kwa kusimamia madeni yake.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa mawaka wa 2020/2021 Shirika lilikasimiwa kukusanya jumla ya **Tsh. Bilioni 3.050** kutokana na kodi za nyumba na hadi kufikia Machi tayari Shirika limeshakusanya kiasi cha **Tsh. Bilioni 2.059** sawa na asilimia 68 ya makadirio. Hivyo, ili malengo yakamilike kwa Shirikia lazima Serikali ihakiishe imesimamia ipasavyo makusanyo yake pamoja na kuwawezesha kusimamia kikamilifu kodi za nyumba pamoja kulipwa madeni yote wanayodai kwa wapangaji wake.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande wa Wakala wa Majengo Zanzibar kamati inapongeza kwa kuendelea na majukumu yao ya kutoa huduma ya makaazi kwa maafisa wakuu wa Serikali na watumishi wa Umma ; Aidha, wakala wa Majengo ina wajibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya ujenzi na matengenezo ya majengo ya Serikali ili kuhakikisha ubora wa majengo hayo. Mbali na majukumu hayo kamati imebaini Wakala wanakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uhaba wa fedha, upungufu wa wataalamu, uhaba wa vitendea kazi vya kisasa pamoja na ukosefu wa ofisi yakudumu.

***Mheshimiwa Spika;***

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kuwasaidia Wakala wa Majengo kuweza kutatua changamoto zao ili kuweza kufikia malengo waliojipangia. Aidha kamati na

hali ya upatikanaji wa fedha za ruzuku ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi Wakala wameingiziwa shilingi milioni 85.966 ambazo ni sawa na asilimia 23% ya makadirio hali ambayo imepelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hivyo, kamati inaishauri  Serikali kuipatia Wakala wa Majengo ruzuku waliopangiwa kwa mwaka 2021/2022 kwa ukamilifu ili kuweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

***Mheshimiwa Spika;***

Kwa upande wa Ofisi ya Afisa Mdhamin Pemba, katika ziara tofauti ambazo tumezifanya kisiwani Pemba kwa kipindi cha mwaka huu, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri na upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo ambapo inapelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Kamati inashauri Wizara kuzisaidia nkikamilifu Taasisis zake zilizopo kisiwani Pemba kwa kuzipatia vyombo vya usafiri pamoja na vifaa vya kisasa ambavyo vinaendana na wakati. Aidha, kamati inashauri Serikali kuziangalia kwa jicho la huruma Taasisis hizi kwa kuzipatia fedha za matumizi kwa wakati ili kuweza kufanikisha malengo yao waliojipangia.

**HITIMISHO**

***Mheshimiwa Spika;***

Kuhusu Makadirio ya Mapato ya **Tsh**. **Bilioni 1.29** ambayo yamepangwa kwa Wizara hii kwa mwaka 2021/2022 kutoka vyanzo mbali mbali, Kamati inashauri Wizara ihakikishe imesimamia vyema makusanyo yake na yatumike kwa mujibu wa taratibu zinavyoelekeza ikiwa ni pamoja kutumika katika miradi ya maendeleo na uendeshaji wa Taasisi husika zenye kukusanya mapato hayo.

***Mheshimiwa Spika;***

Mipango yote iliyomo katika Bajeti hii ya 2021/2022 haitoweza kutekelezeka ikiwa makusanyo ya mapato hayatafanyika kama ilivyokusudiwa kwa Taasisi zote ambazo zinahusika moja kwa moja na ukusanyaji wa mapato. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati kama zilivyopangwa kwenye Bajeti ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Na mwisho kabisa,** ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, kwa niaba ya Kamati yangu tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie kwa kina Bajeti hii na hatimae waidhinishiwe jumla ya fedha zote zilizopangwa kutumika kwa mwaka wa fedha *2021/2022* kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

***Mheshimiwa Spika;***

*Kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

**Ahsante,**

**………………………..**

**(Hudhaima Mbarak Tahir)**

**Makamu Mwenyekiti,**

**KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**